BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Tisa – Tarehe 16 Mei, 2025
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2025/2026.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

113. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

(a) Kuna vikundi vingapi vya ushirika na uwezeshaji vilivyopatiwa mikopo katika jimbo la Mwanakwerekwe.

(b) Tathmini ya mafanikio iko vipi juu ya kutimia kwa malengo yaliyokusudiwa.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

44. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

    Kwa kuwa elimu ya juu ni suala la Muungano, na kwa kuwa vipo vyombo vinavyosimamia masuala ya elimu ya juu kama vile 'National Council for Technical and Vocational Education and Training' (NACTVET) na 'Tanzania Commission for Universities' (TCU).

    (a) Je, ni kwa namna gani vyombo hivi vinaishirikisha Zanzibar katika utekelezaji wake wa majukumu ya kila siku.

    (b) Je, ni chombo gani kinachotoa miongozo ya usimamizi wa elimu ya juu kwa Wizara ya Elimu kwa upande wa Zanzibar.

    (c) Je, Serikali haioni sasa ni muda muafaka wa kuiondoa elimu ya juu katika suala la Muungano ili Zanzibar iweze kuisimamia elimu ya juu mwenyewe.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

244. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

    Pamoja na umuhimu wa nishati ya umeme katika maisha yetu, huduma hiyo inakabiliwa na changamoto ya kucheleweshwa sana kushughulikiwa kwa nguzo za umeme zinapoanguka katika vijiji na mitaa mbali mbali. Wananchi hutoa taarifa katika Ofisi za Shirika la Umeme la Zanzibar (ZECO) za Wilaya zaidi ya wiki mbili au tatu, lakini watoa huduma wa ZECO hawatoi ushirikiano kwa kuliondoa tatizo hilo katika wakati muafaka.

    Je, linapotokea tatizo la nguzo mwananchi anatakiwa atoe taarifa wapi kwa hatua za haraka za utatuzi.

**Wizara ya Afya:**

140. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Tathmini iko vipi juu ya ongezeko la watoto wanaozaliwa na mgongo wazi.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

108. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kwa kiasi gani Wizara yako inajikita zaidi kuwekeza kwenye tasnia ya tiba utalii katika kuuongezea thamani utalii wetu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa mwaka 2025/2026.

Zanzibar,
16 Mei, 2025.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA